

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 026 23222761-5
Fax No. +255 026 2322624
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Ofisi ya Bunge imesikitishwa na taarifa za uzushi zilizosambazwa kwenye mitandao ya kijamii zikilihusisha Bunge na Waheshimiwa Wabunge na shughuli za Mfuko wa Utoaji Mikopo unaojiita **FOCUS VICOBA**. Barua ya kughushi ikiwa na picha ya Mhe. Jokate Mwegelo, Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, imedai kuwa Ofisi ya Bunge imeidhinisha na kutambua uwepo wa mfuko huo.

Tunapenda kuarifu na kuutahadharisha umma kuwa taarifa hiyo ni ya uwongo yenye lengo la kulichafua Bunge pamoja na kuhalalisha vitendo vya utapeli vinavyofanywa na Asasi hiyo.

Ofisi ya Bunge inakanusha kujihusisha kwa namna yoyote ile na shughuli za Asasi hiyo kwani hilo sio jukumu la msingi la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hivyo, kupitia taarifa hii, Ofisi ya Bunge inatoa onyo kali kwa Asasi ya **FOCUS VICOBA** kwa kitendo cha udanganyifu na uvunjifu wa Sheria za Nchi na kuahidi kuchukua hatua pale itakapobidi.

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,
Ofisi ya Bunge,
S.L.P 941,
DODOMA.

16 Machi, 2021.